
# MASOMO YA BIBLIA KWA WATOTO WA MIAKA 4-6

## MWALIMU

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Kwanza



MARAFIKI
(FRIENDS)

Marafiki, marafiki,
Sisi tu marafiki,
Kwa kucheza kwa furaha.

```
Key D  /s :l/s :s .m' :d/r.m :f :f .s/l .t/
```

YESU ANIPENDA
(JESUS LOVES ME)

Yesu Anipenda,
Yesu Anipenda,
Kweli Anipenda,
Mungu Amesema.

```
Key Eb  /s :m :s :s / .d' :-/s :m
           :d :d/m.r :-l
        /s :m :s :s l/.d' :- .l/s .d
           :m/.r/d :-//
```

YESU NI RAFIKI MWEMA
(MY BEST FRIEND IS JESUS)

Yesu ni rafiki,
Msifuni, msifuni,
Yesu ni rafiki,
Namsifu.

```
Key Bb   s .m :r .m/d :s/r :s/m :s/
         s .m :r .m/d :s/r :s/d :-/
```

NAWEZA KUKUA
(I CAN GROW)

Ninafuraha kujua naweza kukua,
Sijui ni kwa nini?
Mama husema Mungu amepanga hivyo,
Ananitaka niwe mkubwa pia.

```
Key F  s d:d r:r m:f s f m'd r:t t d:l/
       s d:d r:r m:f s:f m:m r:r d:-l-
```



# MASOMO YA BIBLIA

## KWA
## WATOTO WA MIAKA 4-6

## MWALIMU

**Mwaka wa Kwanza** **Kitabu cha Kwanza**

B1-1Ts

Used by permission of International Publications Services

© Copyright 1986
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

## HATUA ZA KUFUATA KATIKA KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

**Hatua ya 1: Jitayarishe mwenyewe kwa maombi.**

**Hatua ya 2: Soma somo lote.**

**Hatua ya 3: Soma kuhusu mkazo wa somo na ufikirie jinsi unaweza kutimiza lengo hilo.**

**Hatua ya 4: Soma maandiko ya Biblia.**

**Hatua ya 5: Jifunze kusimulia hadithi kwa watoto.**

**Hatua ya 6: Jifunze kifungu cha Kukumbuka.**

**Hatua ya 7: Jifunze kuimba nyimbo zilizopendekezwa.**

**Hatua ya 8: Jifunze mpango wa kufundisha somo.**

**Hatua ya 9: Fika mapema Jumapili na utayarishe mahali pa kukutania.**

## HATUA ZA KUFUATA DARASANI MWAKO KILA JUMAPILI

Hatua ya 1: Fika mapema; na utayarishe mahali pa kukutania.

Hatua ya 2: Watoto wanapofika:
Mkaribishe kila mmoja, na umwite kwa jina lake.
Pokea sadaka.
Weka alama kwa kitabu cha rekodi.
Andika kila jina la mtoto katika kitabu.

Hatua ya 3: Kulifundisha somo:
Kila siku utatumia nyimbo, wakati wa maombi, vifungu vya Biblia, anza kusimulia hadithi ya Biblia kwa kitendo. Hata hivyo, utaratibu huu waweza kutofautiana; fuata mpango uliopendekezwa kila wiki.

Kila mara wape watoto nafasi ya kujibu maswali unayouliza na kushirikiana katika mawazo yao.

Hatua ya 4: Wakati watoto wanapoondoka:

Ikiwezekana, mpe kila mtoto karatasi ya kupeleka nyumbani ambayo ina picha ya hadithi ya leo.

DOKEZO: Kama watoto hawafahamu nyimbo zote, wafundishe wimbo mpya kila mwezi. Pia, waweza kutumia nyimbo wanazofahamu.

## NAJUA MUNGU ANANITUNZA (GOD TAKES CARE OF ME I KNOW).

Najua Mungu Ananitunza,
Mchana, na Usiku,
Najua Mungu Ananitunza,
Mungu Ananitunza.

```
Key F   /s  :-  :m/r  :d  :r/m  :-  :f/:m  :m  :-/
        /s  :-  :m/r  :-  :-/s  :m  :m/:m  ;-  ;-/
        /s  :-  :m/r  :d  :r/m  :m  :f/m  :m  :-/
        /r  :m  :f/m  :-  :r/d  :-  :-/-  :-  :-//
```

## NJIA YA FURAHA (THE HAPPY WAY)

Na mpendaane,
Na mpendaane,
Hii ni njia ya Furaha,
Na mpendaane.

Na msaidiane,
Na msaidiane,
Hii ni njia ya furaha,
Na msaidiane.

Na mshirikiane,
Na mshirikiane,
Hii ni njia ya furaha,
Na mshirikiane.

```
Key D   /m  .m  :m  .m/m  :d/s  .s  :s  .s/l  :s/
        /d'  :t.l  / s  .l  :s  .f/m  .m  :s  .m/
        /r  :d//
```

## NISAIDIE KUWA MWEMA (HELP ME TO BE KIND)

Nisaidie kuwa mwema,
Ee Mungu siku yote;
Nisaidie kufanya yale yanipasayo,
Kazini kwangu na michezoni.

```
Key Eb   /s  .s  :l  .s/s  .f  :m/r  :d  .r/m  :-/
         /s  .s  :l  .s/s  .f  :m/r  .r  :m  .r/d  :-/
```

## NYIMBO

**NAPENDA KANISA**
**(I LIKE TO GO TO CHURCH)**

**Na-penda Ka-ni-sa,**
**Na-penda Ka-ni-sa,**
**Na-penda Ka-ni-sa,**
**Na-penda Nyi-mbo twa-im-ba,**
**Na-penda Ka-ni-sa.**

```
Key G   : .s,d.r:m.f s:-.s d.r:m.f s:-.3
        :  f.m:r.f m.f:s.l s.f:m.r d:_.
```

**MSAIDIZI NAKUWA**
**(A HELPER I WILL BE)**

**Msaidizi na kuwa,**
**Msaidizi na kuwa;**
**Tu na kazi,**
**Tu na kazi,**
**Ndani kanisani.**

```
Key F   /:s d :- :d/d- :- - :d/
        /m :- :m m :- :m/m :- :- :- ;m/
        /s :- :s/s :- :ls :- :m/d :- :-/
        /m :- :m/r :- :r/d :- :-/:- :-/
```

**MUNGU YU KARIBU**
**(GOD IS VERY NEAR)**

**Mungu Yu karibu,**
**Mungu Yu karibu;**
**Hutusikia tunapo imba na kuomba,**
**Mungu Yu karibu.**

```
Key B   /s :m d :l/t :t - :s/:f/
        /r :t/d :d ; :d/
        /d :/t :l s :m/m :-/l :l/
        /t :s d/ :d -://
```



## YALIYOMO


Hatua za kufuata katika kujitayarisha kufundisha ........ 2

Hatua za kufuata kila Jumapili darasani mwako ........ 2

**LENGO LA 1: MARAFIKI WA KANISA**

**LENGO LA 1: MARAFIKI WA KANISANI**


**Kusudi:** Kumwongoza kila mtoto katika kufanya kazi na kushiriki na marafiki kanisani.

Rafiki wa mtoto ni yule ambaye anampenda. Rafiki wa mtoto ni yule ambaye anafanya kazi naye na kucheza naye.

Kusudi la hatua hii ni kwa mtoto, mchungaji na mwalimu kuwa rafiki wa kila mmoja. Huwa marafiki wanapofanya kazi, wanapocheza na kushiriki pamoja.


Somo la 1 Yesu na Waalimu ........ 4
Somo la 2 Paulo na Rafiki yake, Timotheo ........ 6
Somo la 3 Paulo na Lidia ........ 8
Somo la 4 Samweli Asaidia Kanisani ........ 10

**LENGO LA 2: MUNGU ANATUTUNZA**


**Kusudi:** Kumwongoza kila mtoto aelewe kuwa Mungu anamtunza.

Watu wote wanatakiwa kujua kwamba kuna mtu anayewatunza. Watoto wengi hawajui kwamba Mungu huwatunza kila wakati na mahali popote walipo.

Vifungu vya Biblia, hadithi na nyimbo zilizomo katika somo hili, vitawasaidia watoto kuelewa kuwa Mungu anawatunza.


Somo la 5 Yesu Afundisha Kuhusu Ulinzi wa Mungu ........ 12
Somo la 6 Safari ya Yakobo ........ 14
Somo la 7 Dhoruba Kuu ........ 16
Somo la 8 Jemadari Naamani Alipokuwa Mgonjwa ........ 18

**LENGO LA 3: MUNGU HUWAPANGIA WATOTO KUKUA**


**Kusudi:** Kumwongoza kila mtoto afahamu kwamba Mungu amempangia akue.

Kukua ni sehemu ya mpango wa Mungu. Miili ya watoto hukua. Akili nazo hujifunza mambo mapya. Hujifunza kucheza na watoto wengine. Hujifunza kuhusu Mungu. Mwalimu anaweza kuwasaidia kukua katika kila sehemu.

Mwalimu anaweza kuwasaidia watoto kufanya kazi, kucheza na kushiriki pamoja wanapokua.


Somo la 9 Chakula Chema kwa Danieli ........ 20
Somo la 10 Jinsi Ukuta Ulivyojengwa ........ 22
Somo la 11 Chakula Cha Mchana Cha Mvulana ........ 24
Somo la 12 Daudi na Mtu Kilema ........ 26
Somo la 13 Msamaria Mwema ........ 28

**Nyimbo za Kutumia** ........ 30



Somo 1

# YESU NA WAALIMU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mwalimu ni rafiki wa kila mtoto.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "...Na twende nyumbani kwa Bwana." (Zaburi 122:1).

Nyimbo:
"Yesu ni Rafiki Yangu Mwema"
"Napenda Kwenda Kanisani"

Tumia picha Namba 1.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Luka 2:40-52

Yesu alipelekwa hekaluni huko Yerusalemu alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili. Mle hekaluni alikutana na waalimu na kuzungumza nao. Waalimu walipendezwa na Yesu. Kumbuka kwamba unataka kuwafundisha watoto katika darasa lako kuwa, mwalimu wao ni rafiki wao.

Yesu alikulia katika nyumba ya Kiyahudi. Alifundishwa Biblia. Alijifunza nyimbo na kuomba. Alipofikia umri wa miaka sita, alienda shuleni katika sinagogi. Pia, alienda kuabudu katika sinagogi iliyoko kijijini mwao. Maria na Yusufu walienda pamoja naye kila juma. Alipokuwa na umri wa miaká kumi na miwili walisafiri hadi Yerusalemu kuabudu. Walienda wakati wa sikukuu ya Pasaka. Hii ilikuwa siku maalum kwa Wayahudi. Ilikuwa siku ya kukumbuka vile Mungu aliwaokoa watu huko Misri. Soma hadithi hii katika Kutoka 12.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. MAKARIBISHO: Msalimie kila mtoto anapofika darasani.
2. Wimbo: "Yesu ni Rafiki Yangu Mwema"
3. Sadaka: Waulize watoto kufika na kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka.
4. Maombi: Mshukuru Mungu kwa vipawa ambavyo watoto wametoa.
5. Rekodi: Andika jina la kila mtoto katika kitabu. Weka alama (✓) kama amehudhuria. Fanya hesabu ya watoto.
6. Sema: "Nina rafiki. Mngependa kujua jina lake? Rafiki yangu ni ____________ (taja jina la mtoto mmoja darasani) Je, ungependa kuja na kukaa karibu nami, __________ ? Je, una rafiki? Jina lake ni nani? ____________ Unaye rafiki? Jina lake ni nani? Sisi



5. Ita kila jina na uweke alama (✓) kwa wale waliohudhuria. Shukuria wale ambao wamehudhuria kila Jumapili kwa miezi mitatu.
6. Imba: "Hivi ndivyo jinsi na fagia sakafu, na fagia sakafu, na fagia sakafu. Hivi ndivyo jinzi na fagia sakafu kila asubuhi ya Jumapili." Fanya kitendo hicho unapoimba. Vifungu vingine ni, "Hivi ndivyo jinsi napangusa kiti; na nawa uso, naenda kanisani." (Tumia sauti yo yote unayopenda).
7. Uliza, "Je, mtu yoyote alikusaidia asubuhi ya leo? Ni nani aliyekupikia chai? Ulikuja pamoja na nani kanisani?" Wasaidie watoto waelewe kuwa wenzao waliwasaidia.
8. Somo letu la leo ni kuhusu msaidizi. **Fungua Biblia yako katika Luka 10** na usimulie hadithi.

**MSAMARIA MWEMA**

Siku moja, mtu mmoja alisafiri kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko. Alikuwa ametembea mahali parefu. Kwa hivyo, alitembea haraka kwa kuwa usiku ulikuwa unakaribia. Alijua kuwa njia hiyo haikuwa na usalama. Alikuwa ameambiwa kuwa mara kwa mara wanyang'anyi hujificha katika miamba iliyoko kando ya barabara. Alipokuwa akijiharakisha, watu fulani walitokezea nyuma ya mwamba mkubwa. Wakampiga msafiri huyo na kuchukua pesa zake pamoja na nguo. Wakamwacha barabarani.

Alijeruhiwa sana na akawa karibu kufa. Akamsikia mtu akitembea. Akafikiria, "Mtu anakuja, naye atanisaidia." Lakini mtu huyu hakusimama. Alitembea kwa haraka na kupapita mahali hapo. Alikuwa kuhani ambaye alikuwa na kazi ya kufanya huko Yeriko.

Baadaye kidogo, yule mjeruhiwa alimsikia mtu mwingine akija. Akajiambia moyoni, "Mtu anakuja. Kwa hakika atanisaidia." Lakini mtu huyu hakusimama kamwe. Aliogopa pengine angevamiwa na wanyang'anyi. Akapitia upande mwingine wa barabara.

Kukawa giza. Yule mjeruhiwa akasikia sauti, "Klip, klop, klip, klop." Sauti hii ilisikika kama hatua za punda akitembea. "Pengine mtu huyu atanisaidia," akawaza hivyo.

Yule mjeruhiwa akasikia sauti, "Nitakusaidia." Mtu yule mgeni akasimama. Akapaka dawa kwa vidonda vya mjeruhiwa yule. Akavifunga.

Halafu mtu yule kutoka Samaria akampandisha mjeruhiwa kwa punda wake. Wakaenda kwa chumba cha kukodisha hotelini. Hapo wakapumzika chumbani na kula chakula.

Kesho yake asubuhi, yule mtu kutoka Samaria alipaswa kuendelea na safari yake. Kwa hivyo, akampa maagizo mtumishi wa hotelini. Akamwambia amtunze yule mjeruhiwa hadi atakapopona. Akamwachia pesa za malipo ya kazi na msaada wake.

9. Waambie watoto kuwa, "Biblia inasema, wakasaidiana kila mtu na mwenzake." Hivi ndivyo Mungu anatutaka tufanye. Hebu na tuseme pamoja kifungu hiki."
10. Imba: "Msaidizi Nakuwa"
11. Uliza, "Wangapi kati yenu walitenda wema katikati ya wiki?" Waache watoto waseme kile walichofanya. Watie moyo wawasaidie watu wengine wiki ijayo.
12. Omba, "Asante Mungu kwa kutuwezesha kuwasaidia wengine."
13. Wimbo: "Njia Ya Furaha"



Somo 13

# MSAMARIA MWEMA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Watoto wanaweza kusaidia wengine.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Wakasaidiana kila mtu na mwenzake"(Isaya 41:6).

Nyimbo:
"Njia Ya Furaha"
"Msaidizi Nakuwa"
Tumia picha Namba 13.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Luka 10:30-37.

Ukweli ambao unapaswa kusisitizwa ni kwamba Msamaria ndiye aliyewasaidia wengine.

Mtu mmoja, ambaye alikuwa Myahudi, alikuwa akisafiri kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko. Njia hii ilikuwa mbaya sana. Kila wakati wanyang'anyi walijificha katika pango na miamba iliyokuwa karibu na njia hiyo. Mtu huyu akashambuliwa na wezi. Wakampiga na kumnyang'anya nguo zake. Wakamwacha amelala kando ya barabara karibu kufa.

Watu watatu walipitia mahali pa tukio hiyo. Wa kwanza alikuwa kuhani. Alikuwa mtumishi wa Mungu. Alimtazama mjeruhiwa yule na kwa haraka akampita.

Mtu wa pili alikuwa Mlawi. Alikuwa kiongozi kanisani, lakini aliogopa kusimama. Hakumsaidia mjeruhiwa yule.

Mtu wa tatu alikuwa akitoka Samaria. Wayahudi hawakuwapenda Wasamaria. Hata hivyo, Msamaria huyu alimsaidia Myahudi aliyekuwa amejeruhiwa.

Yesu alitumia hadithi hii kumfundisha wakili kuwa jirani mwema kwa wengine. Yesu alimwamuru wakili yule aende na kuwa mwema kama alivyokuwa yule Msamaria kwa mtu yule aliyepigwa na wanyang'anyi.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika na uwaache wakusaidie kupanga na kutayarisha chumba.
2. Wimbo: "Msaidizi Nakuwa".
3. Maombi: "Asante Mungu kwa kanisa letu. Asante kwa jua (au mvua). Tusaidie tujifunze zaidi kuhusu wewe."
4. Waulize watoto kutoa sadaka zao, sema, "Tunaweza kusaidia kanisa letu tunapotoa sadaka. Tunaweza kununua vitabu vya shule ya Jumapili, viti na vitabu vya nyimbo."



wote tunaye rafiki maalum. Mnajua jina lake? Tumeimba kuhusu yeye...Yesu. Hebu tusimame na tuimbe."

7. Wimbo: "Yesu ni Rafiki Yangu Mwema."
8. Somo la Biblia: Sema, "Yesu alipokuwa kijana alienda kanisani. Alijifunza kifungu cha Biblia katika Zaburi: '...Na twende nyumbani kwa Bwana.' (Zaburi 122:1) Sikilizeni ninapokisoma kutoka Biblia. Semeni ninavyo soma."
9. **Fungua Biblia Yako Katika Injili ya Luka 2:40** na usimulie hadithi:

**YESU NA WAALIMU**

Yesu alipenda kwenda kanisani. Alienda pamoja na Maria na Yusufu kila juma. Alikuwa na marafiki wengi kanisani.

Siku moja asubuhi aliamka mapema. Kulikuwa bado ni usiku. Lakini alisikia kelele jikoni. Aliuliza, "Mama, unafanya nini?" Maria akasema, "Yesu, umesahau? Leo ni siku muhimu. Tunaenda Yerusalemu."

Yesu alikuwa mwenye furaha. Alisaidia kwa matayarisho ya safari. Wakaweka matunda na mikate katika vikapu. Halafu wakamwekelea punda mizigo hiyo. Baadaye, safari ikaanza.

Marafiki wengine walisafiri nao. Watu wengi walienda Yerusalemu. Maria alitembea pamoja na wanawake na hata watoto wadogo. Yesu na marafiki zake walikuwa wenye furaha. Waliimba nyimbo; wakacheza michezo; wakakimbizana na kusemezana. Yusufu na wazee wengine walitembea nyumba ya jamaa zao. Usiku watu wote walisimama na kupumzika.

Siku iliyofuata, mtoto mmoja mvulana alisema, "Naona Hekalu" Lilikuwa jengo ndefu nyeupe. Kilele chake kilionekana juu ya nyumba zote. Yesu na marafiki zake walishangaa sana.

Yesu na jamaa yake walipanda hatua za kuingia hekaluni. Waliwasikia wana kwaya wakiimba. Waliwasikia waalimu wakisoma Biblia. Yesu alisimama na kuwasikiza. Aliuliza maswali. Waalimu walizungumza na Yesu. Walistaajabia ufahamu wa Yesu. Wakasema, "Je, ni jinsi gani kijana huyu anajua mambo mengi kuhusu Neno la Mungu?" Yesu alikaa na kuwasikiza. Hakujua wakati wa kwenda nyumbani ulikuwa umefika. Hakuwaona Yusufu na Maria wakitoka hekaluni.

Waliporudi wakimtafuta, Yesu alikuwa angali anawasikiza waalimu. Yusufu akasema, "Njoo, Yesu, ni lazima twende nyumbani." Kwa hivyo, Yesu aliwaacha waalimu na kwenda nyumbani pamoja na Maria na Yusufu. Alikuwa na marafiki wapya huko hekaluni. Waalimu walikuwa marafiki wa Yesu.

10. Wimbo: "Napenda Kwenda Kanisani"
11. Picha: Waonyeshe watoto picha namba 1. Uliza watoto: "Mnamwona nani katika picha hii? Je, mwalimu anafanya nini? Mnafikiri mwalimu anapenda watoto? Mwalimu ni rafiki wao. Hebu na tumshukuru Mungu kwa ajili ya marafiki.
12. Maombi: Omba, halafu umpe kila mtoto picha ya kupeleka nyumbani.



Somo 2

# PAULO NA RAFIKI YAKE TIMOTHEO

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mchungaji ni Rafiki wa watoto.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Rafiki hupenda sikuzote" (Mithali 17:17).

Nyimbo:

"Yesu ni Rafiki Yangu Mwema"
"Napenda Kwenda Kanisani"

Tumia picha Namba 2.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Matendo 16:1-3

Paulo alikuwa mhubiri mwenye juhudi. Alikuwa rafiki wa kijana mmoja, Timotheo. Alimsaidia Timotheo. Huu ni mfano wa urafiki ambao ulianzia kanisani.

Paulo alisafiri hadi miji mbalimbali. Alihubiri katika vijiji vingi. Alienda mjini ambako Timotheo na jamaa yake waliishi. Timotheo alikuwa angali kijana mdogo. Yeye na jamaa yake walimsikia Paulo akihubiri.

Mama yake Timotheo aliitwa Eunike na nyanya yake aliitwa Loisi. Wote walikuwa Wakristo. Baba yake hakuwa Mkristo. Kwa hivyo, mama yake Timotheo alimfundisha. Alimwamini Yesu kama Mwokozi wake.

Baada ya miaka kupita, Paulo alirudi Listra na akamwona Timotheo. Timotheo alikuwa mwaminifu katika kazi yake kwa Yesu Kristo. Paulo alimwuliza Timotheo kwenda naye katika safari yake ya kuhubiri. Timotheo alijifunza mambo mengi kutoka kwa Paulo. Timotheo alimheshimu na kumpenda Paulo.

Yampasa mchungaji wa kanisa lako kuwa rafiki wa watoto. Wanamheshimu na wanampenda.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Sema: "Nina furaha kuwaona marafiki zangu leo. Nina furaha kuwa kanisani. Je, nanyi mna furaha? Hebu na tuimbe wimbo wa furaha."
2. Imba: "Napenda Kwenda Kanisani."
3. Mwulize mtoto mmoja kuchukua chombo cha kuweka sadaka. Waambie watoto waweke sadaka zao humo. Mwulize mtoto huyo kumshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka.
4. Ita jina la kila mtoto na uweke alama ( ) kwa waliohudhuria. Wahesabu watoto.
5. Sema: "Ni nani mchungaji wa kanisa letu? Ndio, ________ ni mchungaji wetu. Anapenda kusikia mkiimba. Mngependa kumwimbia wimbo leo? Hebu sasa



Eleza kuwa unaenda kuiga kitendo cha kuwa mwema. Iga kama unalima shamba. Uliza, "Je, ninafanya nini?" Halafu waambie wengine kuiga kitendo cha kuwa wema: kubeba maji, kuosha vyombo, kufagia na kadhalika. Vitendo hivi ni vyema kwa sababu twawasaidia wengine.

7. Sema, "Hadithi yetu ni kuhusu mfalme Daudi. Inatwambia kile ambacho Daudi alitenda kilichokuwa chema. **Fungua Biblia yako katika 2 Samweli 9** na usimulie hadithi.

**DAUDI NA MTU KILEMA**

Mfalme Daudi alikuwa amekaa katika nyumba yake kubwa. Akakumbuka alipokuwa kijana. Alikuwa na rafiki aliyeitwa Yonathani. Waliwinda pamoja, waliimba pamoja na hasa walikuwa marafiki.

Mfalme Daudi akamwita mtumishi wake. Akamwuliza, "Jamaa ya Yonathani iwapi? Waweza kunisaidia kuwatafuta?"

Mtumishi mmoja akasema, "Yonathani alikuwa na mtoto mmoja. Aliumizwa alipokuwa mtoto mdogo. Kwa sasa yeye ni kilema. Jina lake ni Mefiboshethi."

"Anaishi wapi?" Daudi akauliza.

"Hana nyumba yake mwenyewe. Anaishi na rafiki yake," mtumishi akajibu.

"Mleteni Mefiboshethi kwangu. Nataka kumsaidia," Daudi akajibu.

Mtumishi yule alikwenda kwa Mefiboshethi na jamaa yake. Akawaleta wamwone mfalme. Daudi akaona kuwa Mefiboshethi alikuwa kilema miguu yote miwili.

"Usiogope," Daudi akasema. "Mimi na baba yako tulikuwa marafiki. Alinisaidia mara nyingi sana. Ninataka niwe rafiki yako, na niwe mwema kwako."

Mefiboshethi aliposikia maneno ya Daudi, hakuogopa tena.

Daudi akasema, "Njoo uishi pamoja nami, na uje na jamaa yako. Utaweza kula pamoja nami kila siku."

'Asante, Mfalme Daudi. Nimefurahi kwa kuwa wewe ni rafiki yangu. Na tena, umenitenda mema."

8. Imba: "Niongoze Niwe Mpole"
9. Maombi: "Asante Yesu, kwa kuwa rafiki yangu. Asante kwa mwalimu wangu ambaye ni mwema na mpole kwangu."
10. Onyesha picha ya Daudi na Mefiboshethi, No. 12. Uliza, "Daudi alikuwa nani?" (Mfalme wa Israeli). "Mefiboshethi alikuwa nani? (Mtoto wa Yonathani). "Daudi alimsaidiaje?" (Waache watoto waseme njia ambazo Daudi alimsaidia nazo mtu huyu kilema.) Ndiyo, Daudi alikuwa mwema na mpole kwa Mefiboshethi. Unaweza kusema njia ambazo tunaweza kuwa wema na wapole kwa watu wengine? Wasaidie watoto kutaja vitu ambavyo wanaweza kufanya kuwasaidia wengine. Sema, "Hebu na tumtendee mtu wema. Je, utafanya nini leo? Kumbukeni kwamba baba na mama zetu huhitaji msaada wetu kila siku."
11. Imba: "Niongoze Niwe Mpole"
12. Mwulize mtoto mmoja aombe. Amwombe Mungu tuwe wema na wapole.



Somo 12

# DAUDI NA MTU KILEMA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Watoto wanaweza kuwa wema au wapole kwa wenzao.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi." (Waefeso 4:32).

Nyimbo:
"Niongoze Niwe Mpole"
"Njia Ya Furaha"

Tumia picha Namba 12.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 2 Samweli 9

Katika hadithi hii, watoto watatambua kuwa Daudi alimhurumia Mefiboshethi. Kusudi la somo hili ni kuwafundisha watoto kuwa wapole na kuwahurumia wenzao.

Wakati Daudi na Yonathani walipokuwa vijana wadogo, walikuwa marafiki. Mfalme Sauli alikuwa babake Yonathani. Mfalme alimwonea Daudi wivu; akajaribu kumwua. Yonathani na Daudi waliahidiana kuwa marafiki kila mara. Daudi akaahidi kuwa rafiki wa Yonathani na rafiki ya watoto wake pia.

Baadaye mfalme Sauli na mwanawe Yonathani waliuawa katika vita. Daudi alihuzunika sana. Alipokuwa mfalme, alikumbuka ahadi yake kwa Yonathani.

Daudi alifahamu kuwa Yonathani ana mtoto mwanaume. Jina lake lilikuwa Mefiboshethi. Alikuwa kilema wa miguu yote miwili. Hangeweza kutembea.

Daudi alitaka Mefiboshethi aletwe katika makao ya kifalme. Daudi alimwonea huruma. Akampa mashamba yote ya babu yake, Sauli. Akamwalika Mefiboshethi kula pamoja naye katika maisha yake yote yaliyobaki.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto. Waite kwa majina yao unaposema nao.
2. Imba: "Njia Ya Furaha"
3. Omba, "Asante Mungu kwa ajili ya marafiki. Asante Mungu kwa kanisa na kwa baraka zako zote ulizotupatia.
4. Sadaka: Imbeni wimbo wa "Njia Ya Furaha" watoto waletapo sadaka zao.
5. Ita jina la kila mtoto na uweke alama kwa wale waliohudhuria.
6. Waambie watoto kwamba kifungu cha leo cha Biblia chasema, "Tena, Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi."



na tuimbe, na baadaye tutamwalika aje kutusikiza.

6. Imba: "Yesu ni Rafiki Yangu Mwema."
7. Sema: "Napenda kuja kanisani. Je, mnapenda kuja? Sisi hufanya nini kanisani? Ndio, huimba, husoma Biblia zetu, huomba, humsikiliza mchungaji. Yeye ni rafiki yetu. Kuna kifungu ambacho hutuambia yale rafiki afanyayo. "Rafiki hupenda sikuzote" (Mithali 17:17). Waulize watoto kukisema kifungu hiki pamoja.
8. Sema: "Katika Biblia tunasoma kuhusu mhubiri fulani ambaye alikuwa na rafiki maalum." **Fungua Biblia Yako Katika Matendo 16:1-3** na usimulie hadithi.

### PAULO NA RAFIKI YAKE TIMOTHEO

Paulo alikuwa mhubiri. Alisafiri hadi kwa miji mingi. Kila Jumapili alienda kanisani; alipenda kuhubiri.

Siku moja alifika mjini ambako Timotheo aliishi. Timotheo alikuwa angali kijana. Alipenda kwenda kanisani. Alipenda kumsikiliza mhubiri. Alipenda kumsikiliza mhubiri Paulo. Paulo alimwambia mambo mengi kuhusu Yesu.

Mama yake Timotheo alimkaribisha Paulo nyumbani kwao. Alimtayarishia chakula. Paulo na Timotheo waliongea na wakawa marafiki. Timotheo alimwuliza Paulo maswali kuhusu kazi yake.

Paulo aliongea na mama yake Timotheo pamoja na nyanya yake. Paulo aliwaambia kuhusu rafiki yake Yesu. Baadaye Paulo alisafiri hadi kwa mji mwingine kuhubiri. Alimwambia Timotheo kwamba angerudi.

Paulo aliporudi alienda nyumbani kwa Timotheo. Timotheo alikuwa mwenye furaha kumwona rafiki yake. Paulo alimwambia kuhusu safari yake. Waliongea kuhusu rafiki yao Yesu.

Paulo akauliza, "Ungependa kuwa msaidizi wangu? "Ndio," alijibu Timotheo. Ningependa kuwaambia watu kuhusu habari ya Yesu."

Timotheo na Paulo walisafiri hadi miji mbalimbali. Waliwaambia watu wengi kuhusu Yesu. Waliwaambia akina mama na akina baba kuhusu Yesu. Waliwaambia vijana kuhusu Yesu. Waliwaambia wavulana na wasichana kuhusu Yesu.

Timotheo alifurahi kwa sababu Paulo alikuwa rafiki yake. Alifurahi kwa sababu Paulo alikuwa amemwambia kuhusu Yesu. Paulo alikuwa mhubiri na Timotheo alikuwa bado kijana. Paulo alimpenda Timotheo, alifundisha habari za Yesu. Walikuwa marafiki wema.

9. Sema: "Leo mchungaji wetu anakuja kututembelea. Nani ataenda kumwambia kuwa tuko tayari kumkaribisha leo?" Mtume mtoto mmoja akamwite mchungaji. Mnapongojea, wakumbushe watoto wawe wenye heshima na wenye upendo kati yao na mchungaji anapowatembelea.
10. Wakati mchungaji atakapofika sema, "Mchungaji, watoto wetu wangependa kukuimbia. Tunataka ujue kwamba sisi ni rafiki zako na tuna furaha kwa sababu wewe ni rafiki yetu pia. Je, watoto, kunaye mmoja kati yenu ambaye angependa kumwambia kitu mchungaji wetu?"
11. Mwimbieni mchungaji wimbo wa "Yesu ni Rafiki Yangu Mwema".
12. Waonyeshe watoto picha No. 2. Zungumza juu yake.
13. Mshukuru Mungu kwa ajili ya mchungaji na kuwatembelea kwake.



Somo 3

# PAULO NA LIDIA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Watoto hukutana na marafiki kanisani.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Ninyi mmekuwa rafiki zangu" (Yohana 15:14)

Nyimbo:

"Napenda Kwenda Kanisani"
"Yesu ni Rafiki Yangu Mwema"
"Marafiki"

Tumia picha Namba 3.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Matendo 16:13-15

Paulo alitembelea miji mingi. Alihubiri katika makanisa mengi ya miji hii. Somo letu la leo latufundisha kuhusu rafiki maalum wa Paulo.

Paulo alisafiri na rafiki zake, Luka, Sila na Timotheo. Soma Matendo 16:8-12. Roho Mtakatifu aliongea na Paulo. Aliwaongoza hadi Makedonia. Akawaongoza hadi mji wa Filipi. Paulo alienda huko kuwaambia Wayahudi kuhusu Yesu.

Hakukuwa na Wayahudi wengi mjini humo, kwa hivyo hapakuwa na kanisa. Watu walikutanika karibu na mto kwa mahubiri. Paulo na marafiki zake walienda pale na kukutana na watu.

Biblia inatuambia kwamba baadhi ya wanawake walikuwepo hapo mtoni. Mmoja kati ya wanawake hao aliitwa Lidia. Alikuwa mfanya biashara. Aliuza nguo. Kabla ya kuja huko Filipi, aliishi katika mji mwingine. Huko alijifunza kumwabudu Mungu. Katika Filipi alikutana na kuabudu na waamini wengine.

Paulo alihubiri kuhusu Yesu. Lidia alisikiza tu. Alimwamini Yesu kama Mwokozi wake. Pia, jamaa yake walimwamini Yesu.

Lidia alimkaribisha Paulo na marafiki zake kuishi kwake nyumbani wakati walipokuwa huko Filipi.

Wasaidie wanafunzi kufahamu kwamba wanao marafiki kanisani.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika. Sema, "Karibu rafiki yangu ________ " au ________ ni rafiki yangu, nina furaha umefika." Waite watoto kwa majina yao jinsi uwezavyo.
2. Wakati watoto wanapopeleka sadaka zao katika chombo cha sadaka imbeni wimbo huu: "Napenda Kwenda Kanisani".
3. Ita jina la kila mtoto na uweke alama (✓). Hesabu watoto.



kikapu mkononi mwake. Kikapu hiki kilikuwa na chakula chake.

Kijana huyu akaona kusanyiko au kundi la watu wengi. Aliwaona akina baba na akina mama. Aliwaona wavulana na wasichana, pia. Wote wakimsikiliza Yesu. Yesu alikuwa akiwafundisha kuhusu upendo wa Mungu.

Kijana huyu akamwona Yesu ameukalia mwamba, naye akakaa kumsikiliza. Baadaye akawa na njaa. Akakumbuka chakula kilichomo kikapuni mwake, akachukua.

Halafu akamsikia Yesu akisema na Filipo, msaidizi wake. "Watu wana njaa," akasema Yesu. Hatuwezi kuwaambia warudi nyumbani kabla ya kula chakula. Ni lazima tuwalishe."

Filipo akasema, "Kuna watu wengi hapa. Hatuwezi kununua chakula cha kuwatoshea wote."

Kijana huyu alifikiri kuhusu chakula alichokuwa nacho. Kilikuwa cha kutosha mtu mmoja tu! Lakini angemgawia Yesu pekee. Akamkimbilia Andrea, mmoja wa wasaidizi. Akasema, "Nitawagawia chakula changu. Nina mkate na samaki." Andrea akacheka kidogo, kwa kuona kuwa mkate huo na samaki vyatosha kwa kumlisha mtoto mdogo mmoja tu. Lakini alimpelekea Yesu chakula hicho. Akasema, "Yesu, kijana huyu anachakula." Anao mkate na samaki. Lakini havitatosha watu hawa wote."

Yesu akamwambia, "Waambie watu wakae chini." Akachukua mkate na samaki huyo. Akaomba, "Asante sana, Mungu, kwa mkate na samaki hawa."

Yesu akakigawa chakula. Akawaambia wasaidizi wake wampe kila mtu chakula.

Kila mmoja akala jinsi alivyotaka. Baadaye wasaidizi wa Yesu wakakusanya mabaki ya chakula.

Kijana huyo alikimbilia nyumbani huku akiwa mwenye furaha. Alikuwa ameshirikiana chakula chake na Yesu. Yesu aliwalisha watu wengi sana nacho.

6. Sasa gawa mkate ulioleta katika vipande vidogo vidogo na umpatie kila mtoto. Mchague moto mmoja amshukuru Mungu kabla ya kula.
7. Imba: "Niongoze Niwe Mpole".
8. Chagua mtoto mmoja afungue Biblia katika 1 Yohana 4:7. (Weka kijikaratasi mapema kuonyesha mahali hapo). Soma maneno hayo. Mwambie kila mtoto aseme kifungu hiki kwa mwenzake.
9. Sema, "Njia nyingine ya kushirikiana kwa vitu tulivyo navyo ni kwa kutoa sadaka zetu." Asante Mungu kwa sadaka. Mchague mtoto mmoja ashike chombo cha sadaka wakati watoto wanapoendelea kutoa sadaka zao.
10. Imba: "Msaidizi Nakuwa"
11. Picha: Waonyeshe picha No. 11 ya mvulana na chakula chake cha mchana. Uliza, "Mnafikiri Yesu angefurahi kama kijana angejiwekea tu chakula chake? Mvulana huyu alikuwa na nini kikapuni mwake? Je, watu walifurahi? Kwa nini mvulana huyu alishirikiana katika chakula chake? (Alimpenda Yesu). Je, ni vitu gani ambavyo twaweza kushirikiana kwavyo leo?
12. Omba: "Asante Mungu kwa ajili ya marafiki. Asante kwa chakula. Asante kwa kunipenda."



Somo 11

# CHAKULA CHA MCHANA CHA MVULANA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Watoto wote wanaweza kushirikiana.

**Kifungu cha Kukumbuka:**
"Tupendane" (1 Yohana 4:7).

Nyimbo:
"Njia ya Furaha"
"Msaidizi Nakuwa"
"Niongoze niwe Mpole"

Tumia picha Namba 11

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mathayo 14:15-21; Yohana 6:1-13.

Hadithi hii inajulikana sana. Kijana mdogo alikuwa na chakula. Alikuwa na mikate mitano na samaki wawili. Mkate wa aina hii ulitengenezwa kwa shayiri ndio uliokuwa na bei ya chini. Chakula hiki kilitosha kwa mtoto mmoja pekee.

Yesu alichukua chakula hiki na kuwalisha watu wengi sana. Mathayo anasema kuwa wanaume 5000 zaidi ya wanawake na watoto waliolishwa.

Mwujiza ulikuwa na lengo kuliko kutimiza tu mahitaji ya watu. Ulikuwa na ishara za kufundisha watu kuwa Yesu ni nani hasa.

Kijana huyu mdogo alikuwa na moyo wa kushirikiana chakula chake na wenzake. Yesu alitumia mtoto huyu kufundisha watu.

Watoto hujifundisha kushirikiana na wenzao waonapo jinsi wenzao wanavyo shirikiana. Watoto wa darasa lako watajifunza kushiriki wanaposhirikiana.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Kila mara fika mapema ili umsalimie kila mtoto anapofika.
2. Wimbo: "Njia Ya Furaha"
3. Ita kila jina na uweke alama (✓) kwa jina la yule aliyehudhuria.
4. Maombi: "Asante, Mungu, kwa chakula. Asante Mungu kwa kutupatia vile ambavyo twahitaji kila siku."
5. Sema, "Somo letu la leo ni kuhusu kijana mdogo aliyemsaidia Yesu." **Fungua Biblia yako katika Mathayo 14** na usimulie hadithi.

## CHAKULA CHA MCHANA CHA MVULANA

Siku moja kijana mdogo alikuwa akitembea barabarani. Alikuwa na



4. Kabla ya kwenda kanisani, weka vijikaratasi katika Biblia yako kuonyesha vifungu hivi: Mithali 17:17, Yohana 15:14, 2 Wakorintho 1:24, Waefeso 4:32. Yapaswa karatasi hizi ziwekwe ili watoto waweze kuziona.
5. Mwulize mtoto mmoja kuja kuchagua kijikaratasi kimoja. Sema, "Nimeweka kijikaratasi katika Biblia kuonyesha kifungu kinachotuambia kuhusu marafiki. Nitasoma kifungu ambacho ________ amechagua." Soma kifungu hicho. Waulize watoto wengine watatu, mmoja baada ya mwingine, kuja na kuchagua kijikaratasi. Soma kila kifungu. Halafu sema, "Hebu na tuimbe wimbo kuhusu marafiki."
6. Wimbo: "Marafiki"
7. Sema, "Hapo zamani palikuwepo na marafiki ambao hawakuwa na kanisa la kuabudia wala kuimba. Marafiki hawa walifanya ibada karibu na mto. Leo tunaenda nje kuabudu kama vile hao marafiki walifanya." (Waongoze watoto katika msitari, mmoja, mmoja hadi nje. Kaeni kwa manyasi).
8. **Fungua Biblia Yako Katika Matendo 16:13-15** na usimulie hadithi.

## PAULO NA LIDIA

Lidia na marafiki zake walitaka kwenda kanisani. Kwa vile hapakuwa na jengo, walitembea hadi mtoni. Walikaa kivulini karibu na mto. Waliimba; wakaomba; na wakamwabudu Mungu.

Siku moja wanawake walikutana kuabudu. Walimsifu Mungu na kuimba nyimbo.

Siku hiyo wanaume wanne walifika mtoni. Hao pia, walifika kuabudu. "Jina langu ni Paulo," mmoja wao akasema. "Watu hawa wengine ni marafiki zangu: Luka, Sila na Timotheo. Tumekuja kuwaambia kuhusu Yesu, Mwana wa Mungu."

Lidia akasema, "Tumefurahi kwamba umefika. Tumekuwa tukimwomba Mungu atume mhubiri. Jina langu ni Lidia. Hawa ni marafiki zangu."

Wanawake hao walimsikiliza Paulo akihubiri. Aliwaambia kuhusu Yesu. Alisema kuwa Yesu ni rafiki wa kila mmoja. Wanawake hao walifurahi sana kujifunza zaidi kuhusu Yesu. Lidia akamkubali Yesu kama Bwana wa maisha yake.

9. Sema: "Nani anayeweza kuniambia jina la mmojawapo wa marafiki wa Paulo? Lidia, Luka, Timotheo na Sila walikuwa marafiki zake. Je, Ni nani aliyekuwa rafiki wa Lidia? Ndio, Paulo alikuwa na pia wale wanawake, lakini hatujui majina majina yao.
10. Picha: Waonyeshe picha No. 3. Uliza, "Mtu huyu ni nani? (Paulo) Anawaambia nini hao wanawake? (Ya kwamba Yesu ni rafiki yao) Yeye pia ni rafiki yetu. Hebu na tumshukuru Mungu kwa ajili ya marafiki zetu." Uliza: "Je, kanisa ndipo mahali pekee ambapo tunaweza kuwa na Yesu?" (La, yeye huenda nasi kila mahali).
11. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya marafiki. ("Asante Mungu, kwa ajili ya marafiki zetu.")
12. Wimbo: "Yesu ni Rafiki Yangu Mwema".



**Somo 4**

# SAMWELI ASAIDIA KANISANI

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Kila mtoto anaweza kusaidia marafiki kanisani.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Fanya kazi kwa mikono yenu wenyewe" (1 Wathesalonike 4:11).

Nyimbo:
"Marafiki"
"Msaidizi Nakuwa"

Tumia picha Namba 4.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 1 Samweli 1-3

Samweli alikuwa kijana mdogo aliyesaidia hekaluni. Watoto wa darasa lako watajifunza kuwa Samweli alimsaidia mhubiri aitwaye Eli. Eli alikuwa rafiki wa kijana huyu. Watoto wanaweza kusaidia kufanya mambo mengi kanisani.

Hana alikuwa mke wa Elkana. Hakuwa na watoto. Alihuzunika sana; nyumba yao haikuwa ya furaha. Ilikuwa muhimu kuwa kila mwanamke awe na mtoto.

Ilikuwa ni desturi ya jamaa kwenda Shilo kuabudu mara moja kwa mwaka. Mahali hapa palikuwa na hekalu kubwa.

Wakati Hana alipoenda hekaluni kuomba, aliweka ahadi kwa Mungu. Kama Mungu angemjalia apate mtoto mvulana, angempatia Mungu huyu mtoto. Mungu aliyajibu maombi yake. Alipata mtoto mwanaume. Aliitwa Samweli. Wakati Samweli alipokuwa mkubwa wa kuishi peke yake, mama yake alimpeleka hekaluni. Aliishi na mhubiri, Eli. Eli alimpa Samweli kazi ya kufanya. Alifungua milango kila asubuhi. Alipangusa taa. Alipoendelea kukua, aliongezewa kazi nyingi (madaraka) za kufanya.

Samweli akawa kiongozi wa watu wake. Lakini kwanza aliisikia sauti ya Mungu ikisema naye. (Soma 1 Samweli 3). Alipaswa kumjua Mungu kibinafsi kabla ya kuwa tayari kufanya kazi ambayo Mungu amempangia.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Karibisha kila mtoto anapofika.
2. Imba "Marafiki"
3. Sadaka: "Wakati watoto wanapoimba, waongoze kwa kuweka sadaka zao katika chombo cha kuweka sadaka. Mshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka.



kidogo). Mwulize mtoto mmoja akusaidie. Wekeni mikono yenu chini yake na mwinue. Endelea tu kuwaambia watoto wakusaidie hadi mtakapoiinua. Sema, "Kwa kufanya kazi pamoja tumeweza. Mtu mmoja hawezi kuinua peke yake."

7. Wimbo: "Msaidizi Nakuwa"
8. Uliza, "Je, mnajua kifungu cha Biblia kisemacho kuhusu 'kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe.'" Ni 1 Wathesalonike 4:11. "Ni kazi ya aina gani ambayo twaweza kufanya? Biblia yatwambia kuhusu akina mama, baba na watoto ámbao walifanya kazi pamoja."
9. **Fungua Biblia yako katika Nehemia 3** na usimulie hadithi.

**JINSI UKUTA ULIVYOJENGWA**

Siku moja rafiki alimtembelea Nehemia. "Unakumbuka zile kuta zilizouzunguka mji wa Yerusalemu? Unakumbuka ile milango yake mikubwa iliyowafungia maadui nje?" akauliza.

"Ndiyo naikumbuka," akajibu Nehemia.

"Sasa milango imeteketezwa na kuta zake zimebomolewa," rafikiye akamwambia. "Maadui huja humo mjini kila siku."

Nehemia alihuzunika sana. Akamwomba Mungu msaada. Siku moja Nehemia alikuwa na mfalme. "Mbona umehuzunika, Nehemia? Ni nini kinachokusumbua?" mfalme akauliza.

"Milango na kuta za Yerusalemu zimebomolewa," Nehemia akamwambia mfalme. "Si vizuri kwa jambo hili kutendeka."

"Je, ungetaka kufanya nini?" akauliza mfalme.

"Nataka kujenga upya milango na kuta hizo." Ninahitaji pesa za kununua mawe na vifaa vingine," Nehemia akasema.

"Nitakupatia pesa lakini hutajenga mwenyewe" mfalme akasema.

"Nitatafuta watu wa kunisaidia," Nehemia akasema.

Nehemia akaenda kwa haraka hadi Yerusalemu. Akauliza, "Nani atanisaidia kujenga ukuta na kutengeneza milango?"

"Nitakusaidia," mtu mmoja akajibu.

Mwingine akasema, "Nami pia nitasaidia. Naiweza kazi."

Baadaye watu wengi wakaanza kujenga ukuta. Wakati fulani watu walichoka sana. Hata wakataka kuacha kazi. Lakini Nehemia akawahimiza waendelee na kazi. "Hatuwezi kukamilisha kazi hii kama watu wataacha," Nehemia akasema. "Lazima sote tufanye kazi hata ingawa tumechoka sana."

Watu walifanya kazi kwa muda wa siku kumi. Wakafanya kazi siku ishirini hata mpaka hamsini. Baadaye siku hamsini na mbili zilitimia na hapo kazi ikamalizika.

Wakautazama ukuta na milango yake. Wakafurahi sana kwa kuwa walikuwa wamefanya kazi kwa bidii. Nehemia akasema, "Asante sana ninyi wote. Tumejenga ukuta na milango kwa sababu tumefanya kazi pamoja."

10. Wimbo: "Msaidizi Nakuwa"
11. Picha: Waonyeshe picha No. 10 na uulize maswali kuhusu hadithi hii.
12. Maombi: Omba: "Asante Mungu kwa kazi tufanyayo pamoja."



Somo 10

# JINSI UKUTA ULIVYOJENGWA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Watoto waendeleapo kukua, wanaweza kuwasaidia wengine.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Fanyeni kazi kwa mikono yenu wenyewe" (1 Wathesalonike 4:11).

Nyimbo:
"Msaidizi Nakuwa"
"Njia ya Furaha"

Tumia picha Namba 10.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Nehemia 1:1-6:16

Nehemia alikuwa jamaa ya mateka waliopelekwa Babeli baada ya Yerusalemu kubomolewa miaka 100 iliyopita. Uajemi ilitawaliwa Babeli na Nehemia akafanywa mtumishi wa mfalme. Ilikuwa kazi yake kujaza kikombe cha mfalme na divai na kumpatia. Hii ilikuwa kazi maalum.

Wanaume kutoka Yuda walimtembelea Nehemia. Wakamwambia kuwa kuta za mji zimebomolewa. Milango yake imeteketezwa kwa moto. Nehemia akaomba ruhusa kurudi Yerusalemu kusaidia kujenga upya kuta zake. Mfalme alikubali, na Nehemia akaenda Yerusalemu. Maadui zao walisikia kuhusu kazi hii. Wakapanga kuwashambulia Wayahudi. Hawakutaka hizo kuta kujengwa tena. Wakati Nehemia aliposikia kuhusu mpango huu, aliwapatia watumishi vifaa vya vita. Baadhi ya wafanya kazi walilinda wakati wengine walipokuwa wakiendelea na kazi. Wakaendelea kujenga kuta hizo. Kazi hiyo ilikamilika baada ya siku 52.

Ukweli katika somo hili ambao watoto wapaswa kuelewa ni kuwa Mungu huwapangia watu kufanya kazi pamoja.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika.
2. Imba: "Njia Ya Furaha"
3. Waambie watoto kuweka sadaka zao katika chombo cha kuweka sadaka. Unaweza kusema, "Nina furaha kwa kuwa mmeleta sadaka zenu leo. Pesa zenu husaidia kwa kununua vitu ambavyo sisi hutumia kanisani."
4. Omba, "Asante Mungu kwa vipawa hivi."
5. Ita kila jina katika kitabu cha rekodi na uweke alama kwa wale waliohudhuria.
6. Jaribu kuinua meza au kiti kizito kwa mikono yako. (Huwezi hata



4. Ita jina la kila mtoto na uweke alama (✓) katika kitabu. Tambua wale ambao wamehudhuria kila Jumapili ya mwezi huu. Hesabu watoto.
5. Mchezo: Wasimamishe watoto wawili wakiangaliana. Unaposema "Rafiki yangu, tushikane mikono na tuizungushe pamoja," watashikana mikono na kuizungusha. Halafu sema, "Rafiki yangu hebu turuke pamoja. Rafiki yangu, tupige makofi pamoja. Rafiki yangu nami tutembee pamoja." Watoto watafanya kile kitendo unachosema. "Ni vizuri kuwa na rafiki. Ninaweza kufanya kazi na rafiki yangu pia. Kuna hadithi katika Biblia kuhusu kijana aliyemsaidia rafiki yake."
6. **Fungua Biblia Yako Katika 1 Samweli 1,** na usimulie hadithi.

**SAMWELI ASAIDIA KANISANI**

Samweli aliamka mapema. Alivaa nguo haraka na kula chakula cha asubuhi. Hii ilikuwa ni siku maalum. Alikuwa anaenda kanisani. Alikuwa mwenye furaha. Hana, mama yake, akamwita, "Je, Samweli, uko tayari?

"Ndiyo niko tayari, akajibu." "Tunaweza kwenda sasa?"

Walitembea kwa muda mrefu. Samweli alichoka sana. Mwishowe, wakafika kanisani. Wakaingia ndani. Ilikuwa ya kupendeza sana, tena kubwa. Samweli alishangaa sana.

Akamwona Eli, mchungaji. Eli alikuwa mzee mwenye uso wa huruma. Hana akasema, "Mchungaji Eli, huyu ni mtoto wangu, Samweli. Yeye hunisaidia nyumbani. Anataka sasa kulisaidia kanisa."

Eli akauchukua mkono wa Samweli na kumsalimia. Akasema, "Nina furaha kwa sababu umekuja, Samweli. Utanisaidia kufanya mambo mengi.

Samweli akauliza, "Je, nifanye nini?" Eli alitazama kila mahali. Akasema, "Ninataka mtu wa kupangusa viti. Lazima pia taa zipanguswe. Unaweza kuweka mafuta katika taa. Utafungua milango mikubwa kila asubuhi."

Samweli akasema, "Nitafanya kila kitu, na nitakuwa msaidizi mwema. Wewe ni rafiki yangu na ninataka kufanya kazi nawe."

Kwa kweli, Samweli alikuwa msaidizi mwema.

7. Uliza: "Je, Samweli alifanya nini kumsaidia Eli?" Ninajua kifungu cha Biblia ambacho kinatuambia tuwe wasaidizi.
8. Kifungu cha Biblia: "Fanyeni kazi kwa mikono yenu wenyewe" (1 Wathesalonike 4:11). Waulize watoto kusema kifungu hiki pamoja nawe.
9. Omba. Mshukuru Mungu kwa ajili ya kanisa, mchungaji na viongozi wengine.
10. Wimbo: "Msaidizi Nakuwa"
11. Picha: Waonyeshe picha No. 4. Uliza, "Je, watoto wanafanya nini?"
12. Fanya kitu ambacho watoto wataweza kufanyia kanisa. Waache watambue kile unachofanya: (upanguse viti, ufagie sakafu, uweke vitabu kwenye viti n.k.).
13. Wimbo: "Napenda Kwenda Kanisani"



Somo 5

# YESU ANAFUNDISHA KUHUSU ULINZI WA MUNGU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu anatutunza.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu...... hujishughulisha kwa mambo yenu" (1 Petro 5:6,7).

Nyimbo:
"Yesu Anipenda"
"Napenda Kwenda Kanisani"
"Mungu Ananitunza"

Tumia picha Namba 5.

**Kujitayarisha Kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mathayo 6:25-34

Kila mtoto anahitaji mtu wa kumtunza. Wazazi huwalinda na kuwapatia chakula. Watoto wakubwa husaidia kwa kuwatunza watoto wadogo. Somo hili linatufundisha kuwa Mungu huwatunza wote. Katika Mathayo 6:25-34, Yesu anafundisha kuwa Mungu huwatunza ndege na maua. Lakini, hutunza zaidi watu ambao aliwaumba.

Yesu hasemi kuwa haitupasi kufanya kazi. Anafundisha kuwa tusijisumbue bure. Kama Mungu huwalisha ndege, basi nasi pia atatupatia chakula. Kama anayalisha maua, nasi pia atatulinda.

Yesu anatuambia kwamba tumfikirie Mungu kwanza. Anatupenda, atatunza, na hututimizia mahitaji yetu.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto. Fika mapema kabla yao.
2. Wimbo: "Napenda Kwenda Kanisani"
3. Mwulize mtoto mmoja kuchukua chombo cha sadaka. Watoto wanaweza kufika hapo na kuweka sadaka zao.
4. Mshukuru Mungu kwa baraka anazotupatia. ("Asante Mungu kwa vyote unavyotupatia".)
5. Ita jina la kila mtoto na kuweka alama (✓) kwa wale waliohudhuria. Hesabu watoto.
6. Sema: "Waonyeshe watoto ua na kiota cha ndege. Zungumza kuhusu ua. Uliza, "Je, ni rangi gani? Linanukia vizuri? Je, ni zuri? Linahitaji nini ili likue?" (Jua na mvua).

   Onyesha kiota cha ndege. Uliza, "Ni nani aliyekijenga? Alitumia nini? Zungumza kuhusu vile Mungu hutunza ndege. Halafu



au nyuma yake. "Weka mikono ndani na itingishe." (Mtoto ananyosha mkono wake mbele na kuutingisha). Endelea na, "Weka mguu ndani na utingishe-tingishe." Baadaye imba, "weka mwili ndani." (mtoto anaenda hatua moja ndani ya mviringo na kutoka.)

   Baada ya kumaliza kucheza, waambie watoto wakae chini na kunyamaza.

5. Omba, "Asante Mungu kwa miili yetu. Asante kwa ajili ya miguu kwa kuwa twaweza kukimbia na kucheza. Asante kwa mikono tunayotumia. Asante sana Mungu."
6. Sema, "Biblia yatuambia kuwa Yesu alikua kama mtoto mdogo." Luka 2:40 inasema, "Yule mtoto akakua." Akala chakula kizuri na akawa mkubwa na mwenye nguvu. Hebu na tuseme kifungu hicho.
7. **Fungua Biblia yako katika Danieli** 1 na usimulie hadithi.

## CHAKULA CHEMA KWA DANIELI

Mfalme wa Babeli alitaka wasaidizi maalum. Alitaka wasaidizi wenye nguvu. Alitaka wasaidizi wenye hekima. Siku moja mfalme aliwaita watumishi wake. Akasema, chagueni vijana bora zaidi katika nchi hii. Waleteni waishi nyumbani kwangu. Nataka wasaidizi wangu wawe wakubwa na wenye nguvu. Walisheni vizuri, na mwape vinywaji.

Kijana mmoja, aliyeitwa Danieli alichaguliwa kumtumikia mfalme. Pia, marafiki zake watatu walichaguliwa. Waliishi katika nyumba ya mfalme.

Wakati wa kula watumishi waliwaletea vijana hao chakula. Danieli akakitazama chakula alichopewa. Akakitazama kinywaji. Akamwambia mtumishi, "Hatuwezi kula chakula hiki. Chakula hiki na kinywaji havitufai kula. Tafadhali tupatieni mboga tu tule. Tunaweza kunywa maji badala ya divai?"

Mtumishi alikasirika sana. "Mfalme aliniambia niwape chakula hiki na kinywaji. Lazima mkile la sivyo, mfalme atakasirika sana."

Danieli akasema, "Acha tule mboga za majani na tunywe maji tu kwa muda wa siku kumi. Utaona kuwa tuna nguvu zaidi kuliko vijana wengine."

Kila siku Danieli na marafiki zake walikula mboga za majani. Kila siku wakanywa maji. Siku kumi zikaisha.

Danieli na marafiki zake wakajitokeza mbele ya mtumishi wa mfalme. Mtumishi akasema, "Wewe na rafiki zako mko wenye afya nzuri. Mna nguvu kuliko vijana wengine. Ngozi zenu ni laini. Mboga na maji huwafanya vijana kukua. Mtakuwa wasaidizi wema wa mfalme.

8. Zungumza na watoto jinsi Danieli alivyotunza mwili wake. Je, ni chakula gani alichokula? Mboga, matunda, maziwa, maharagwe na kadhalika.
9. Eleza aina ya chakula na uwaache watoto wafikirie ni chakula gani hicho. Waweza kueleza kuhusu maziwa namna hii: "Nafikiria kuhusu kitu fulani mnachokunywa. Mnahitaji kukinywa kila siku. Kinawasaidia kuwa na mifupa na meno yenye nguvu. Ni cheupe. Je, ni nini hicho?"
10. Imba: "Naweza Kukua"
11. Omba, "Asante Mungu kwa ajili ya miili yetu."



Somo 9

# CHAKULA CHEMA KWA DANIELI

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu anataka watoto wakue.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Yule mtoto akakua" (Luka 2:40).

Wimbo: "Naweza Kukua"

Tumia picha Namba 9.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Danieli 1

Kitabu cha Danieli kina sura kumi na mbili pekee. Hadithi hii ya Danieli inawatia moyo watoto kula chakula chema.

Danieli na marafiki zake walishikwa mateka na kupelekwa katika nchi geni. Kuna mambo mawili muhimu tunayojifunza kuhusu Danieli na marafiki zake. Kwanza walikuwa wamefundishwa vyema nyumbani kwao. Pili, walikuwa na ujasiri wa kutenda lililo jema.

Danieli alikuwa amefundishwa na wazazi wake kumwabudu Mungu. Alikuwa amefundishwa kuwa baadhi ya vyakula havikufaa kuliwa (Mambo ya Walawi 11). Kula vyakula hivi kungekuwa ni kutomtii Mungu.

Danieli na marafiki zake walikata shauri kutokunywa divai na kula chakula cha mfalme. Waliuliza wapewe mboga na maji tu kwa muda wa siku kumi. Wakawa na afya nzuri. Mfalme akaona kuwa Danieli na marafiki zake walikuwa bora zaidi kuliko vijana wengine. Kwa hivyo, walimtumikia mfalme na kupewa kazi ya muhimu sana kufanya.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika.
2. Sadaka: Watoto wanapoweka sadaka zao katika chombo cha sadaka, sema, "Tunapokuwa wakubwa, sisi hujifunza kusaidia wengine. Sadaka zetu zitatumiwa na kanisa kuwasaidia watu wengine."
3. Ita jina la kila mtoto na uweke alama (✓) kwa wale walio hudhuria.
4. Waambie watoto, "Mungu ametupatia miili. Tunakimbia na kucheza. Tunaweza kusikia na kutembea. Tunaweza kuimba. Hebu na tuimbe sasa wimbo mpya.

   Waambie watoto wasimame katika mviringo. Nyoosha mkono mmoja mbele. Imba, "weka mkono ndani, toa mkono nje." (Mtoto aweke mkono wake nje ya mviringo



sema, "Pia, Mungu huwatunza watu. Huwatunza watoto. Sisi ni wa muhimu sana kuliko maua au ndege. Mungu anampenda kila mmoja wetu."

7. Wimbo: "Mungu Ananitunza"
8. Omba, "Asante, Mungu; kwa kututunza."
9. **Fungua Biblia Yako Katika Mathayo 6** na usimulie hadithi.

### YESU AFUNDISHA KUHUSU ULINZI WA MUNGU

Yesu aliukalia mwamba mkubwa mlimani. Watu wengi walikaa karibu naye. Wengine walisimama karibu. Watu walikuja kumsikiza Yesu akifundisha kuhusu Mungu. Wa kina baba na mama walifika kumsikiza. Wavulana na wasichana walifika pia. Watu wengi walisafiri safari ndefu kuja kumsikiza Yesu.

Yesu akasema, "Mungu anawapenda. Mungu amenituma niwaambie kwamba anawapenda. Atawatunza. Anataka mwe wenye furaha."

Yesu aliongea na akina baba na akina mama. Akasema, "Msisumbuke bure kuhusu maji au chakula; msisumbuke bure kuhusu mavazi."

"Mungu husaidia kupata chakula. Hutuletea mvua na jua. Mungu humtunza kila mtu.

Yesu akayaangalia mawingu. Akawaona ndege wakiruka angani. Watu wakatazama angani na kuwaona ndege. Yesu akasema, "Wasikizeni ndege. Wanaimba. Wana viota; hupata chakula. Mungu huwatunza; lakini ninyi mwa muhimu sana kwa Mungu kuliko ndege hawa. Mungu huwatunza pia."

Yesu akaiangalia milima. Akaona maua mengi. Kulikuwa na maua mekundu, meupe na ya majano. Akasema, "Maua yanapendeza sana. Mungu aliyaumba. Huyatunza. Mungu anawapenda zaidi kuliko maua haya. Atawatunza."

Yesu akawaangalia. Akasema, "Mungu anaelewa mnahitaji chakula. Atawasaidia kukikuza chakula. Anajua mnahitaji mavazi. Atawatunza. Aminini Mungu kuwasaidia katika kila jambo."

Watu walikuwa wenye furaha. Watoto pia walifurahi. Walitambua kwamba Mungu anawapenda. Walijua kuwa Mungu atawatunza. Yesu aliwahakikishia kwamba hii ni kweli.

10. Wimbo: "Yesu Anipenda"
11. Waulize watoto kusema kifungu cha Biblia pamoja: "Mungu.... hujishughulisha kwa mambo yenu" (1 Petro 5:6,7).
12. Wapeleke watoto kutembea. Tambua vile Mungu hutunza kila kitu. Ndege wana viota. Mchwa wana mahali pa kuishi. Ng'ombe wana nyasi za kula. Mimea hukua. Mtakaporudi, uliza, "Je, ni vipi ambavyo Mungu hukutunza?" (Mungu ametupatia, Baba, Mama, nyumba, chakula)
13. Wimbo: "Mungu Ananitunza"
14. Picha: Waonyeshe picha No. 5 ya Yesu akisema na watu. Uliza, "Yesu anafundisha nini?"
15. Omba, Umshukuru Mungu kwa ulinzi wake.



Somo 6

# SAFARI YA YAKOBO

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu anatutunza hata usiku.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Hutaogopa hofu ya usiku" (Zaburi 91:5).

Nyimbo:

"Yesu Anipenda"
"Najua Mungu Ananitunza"
"Napenda Kwenda Kanisani"
"Mungu Yu Karibu"

Tumia picha Namba 6.

**Kujitayarisha Kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mwanzo 28

Watoto wanatakiwa kujua kwamba Mungu yu karibu hata usiku. Baadhi ya watoto huogopa wakati wa usiku. Hadithi ya Yakobo yaweza kufundisha watoto kuwa Mungu yu karibu kila mara.

Yakobo alimwibia ndugu yake. Alitoroka kwa kuwa alikuwa mwoga. Alisafiri akielekea Harani. Yakobo alichoka sana. Jua lilipokuchwa alilala. Aliweka kichwa chake juu ya jiwe. Alipokuwa amelala usingizi, aliota. Mungu alisema naye. Mungu akamwambia, "Nchi hii ni yako. Nitakupatia wewe na watoto wako."

Mungu aliahidi kumbariki Yakobo. Akamwambia, "Nitakulinda, na nitakusaidia."

Ingawa Yakobo alikuwa ametenda dhambi, Mungu angali atamlinda. Yakobo alipaita mahali hapo "Betheli," yenye maana ya "Nyumba ya Mungu."

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto. Msalimie kila mtoto kwa kutaja jina lake.
2. Wimbo: "Napenda Kwenda Kanisani"
3. Waulize watoto kufika na kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka. Imbeni wimbo wa kutoa sadaka.
4. Ita jina la kila mtoto na uweke alama (✓) katika kitabu cha rekodi. Hesabu watoto.
5. Mchezo: Chagua mtoto mmoja awe mfano wa jua. Asimame mbele na kushika mikono yake juu ya kichwa chake. Watoto wengine wajifanye kuwa wanacheza au wanafanya kazi. Waache wachague: kucheza mpira, kufagia, kupika, au kufanya kazi shambani. Baadaye jua litakuchwa. Mtoto ateremshe chini mikono yake. Watoto wengine walale chini kama kwamba wana



kuwa mgonjwa na alalie mkeka. Waache wengine wafanye "Usaidizi" kwa kuleta maji, dawa na kadhalika.

7. **Fungua Biblia yako katika 2 Wafalme 5:1-19** na usimulie hadithi.

### JEMADARI NAAMANI ALIPOKUWA MGONJWA

Jemadari Naamani alikuwa kiongozi wa jeshi kubwa. Alikuwa mwenye mamlaka, lakini pia akawa na ugonjwa. Alikuwa na vidonda kwenye mikono yake na miguu. Alikuwa na vidonda mwili wote.

Naamani alikuwa na msichana mfungwa nyumbani kwake. Alimsaidia mkewe kwa kufanya kazi. Huyo msichana alifahamu kuwa Naamani ni mgonjwa.

Mkewe Naamani akasema, "Mume wangu ni mgonjwa sana. Madaktari wameshindwa kumsaidia."

"Mungu aweza kumsaidia." Msichana mfungwa akasema. "Kama Naamani atamwendea nabii Elisha, bila shaka atamsaidia. Elisha anaishi Samaria. Atamwomba Mungu amponye Naamani."

Mkewe Naamani alimwendea haraka mumewe. Akamwambia yale mtumwa wao amemweleza. Naamani akajibu, "Nitaenda Samaria kumwona Elisha. Pengine ataweza kunisaidia."

Wasaidizi wa Naamani wakamletea farasi. Kwa haraka, akaanza safari yake ya kwenda Samaria.

Elisha alisikia kwamba Naamani alikuja Samaria. Alijua kwamba Naamani ni mgonjwa. Elisha akamtuma mtumishi wake amwambie Naamani vile atakavyofanya.

"Mwambie Naamani aende kwa mto Yordani. Mwambie ajichovye kwenye mto mara saba, na Mungu atamponya," Elisha akasema.

Mtumishi alimwendea Naamani. Akamwambia yale Elisha aliyosema. "La," akasema Naamani, siwezi nikajichovya kwenye mto. Nitarudi nyumbani.

Naamani na wasaidizi wake wakaanza safari ya kurudi nyumbani. Wakafika kwa mto Yordani. Mmoja wa wasaidizi akamwambia Naamani, "Nabii Elisha amekwambia jambo rahisi sana la kufanya. Ujichovye kwenye mto mara saba. Hivyo si vigumu."

Kwa hivyo, Naamani akaingia mtoni. Akajichovya mara ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita. Halafu akanawa mara ya saba. Vidonda vyote vilipotea. Ngozi yake ikawa laini. Mungu alikuwa amemponya. Mwanamke mfungwa alimsaidia bwana wake kwa kumwambia kuhusu nabii huyu.

8. Mchezo: Waache watoto waige kuwa Naamani. Wajifanye kuwa wanaenda mtoni na kujichovya mara saba. Hesabu wakati watoto wanapochuchumaa mara saba. Fanyeni mchezo huu mara nyingi.
9. Mwache mtoto mmoja afungue Biblia mahali palipowekwa alama pa Zaburi 34:8. Soma kifungu; "Bwana yu mwema." Semeni kifungu hiki pamoja.
10. Wimbo: "Najua Mungu Ananitunza"
11. Picha: Waonyeshe watoto picha No. 8, na uzungumzie kuhusu kile Naamani anafanya. Waulize watoto kama ilikuwa rahisi kwa Naamani kumtii Elisha. Uliza, "Nani hutuponya? Je, ni dawa au daktari?" Wasaidie watoto kufahamu kwamba Mungu ndiye hutuponya.
12. Omba, ukimshukuru Mungu kwa kutulinda wakati tunapokuwa wagonjwa.



Somo 8

# JEMADARI NAAMANI ALIPOKUWA MGONJWA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu anatutunza wakati tulipo wagonjwa.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Bwana Yu Mwema" (Zaburi 34:8).

Nyimbo:

"Yesu Anasaidia Wagonjwa"
"Najua, Mungu Ananitunza"
"Napenda Kwenda Kanisani"

Tumia picha Namba 8.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 2 Wafalme 5:1-19

Mungu anampenda kila mtu. Hutunza afya ya watu. Tunapokuwa wagonjwa, Mungu hutusaidia kupona. Anataka tuwe wenye nguvu.

Katika 2 Wafalme 5:1-19 twasoma kuwa, Naamani alikuwa Jemadari wa jeshi la mfalme wa Shamu. Alisaidia katika ushambulizi wa Israeli. Alikuwa mwanajeshi mwema. Baadaye, akawa na ugonjwa wa ukoma.

Ukoma ulikuwa ugonjwa mbaya sana. Huko Shamu watu wenye ukoma hawakuambiwa kujitenga na watu wasio nao. Hata hivyo, Naamani alikuwa mgonjwa sana. Soma zaidi kuhusu ukoma katika kitabu cha Mambo ya Walawi 13.

Naamani alikuwa na msichana mtumwa wa kutoka Israeli. Alikuwa amefundishwa na wazazi wake kuhusu Mungu. Alimjua Elisha nabii wa Mungu. Aliamini kwamba Elisha angemponya Naamani. Akamwelezea Naamani kuhusu nabii huyo.

Mungu akamponya Naamani. Mungu alitumia msichana huyu mfungwa na Elisha kumsaidia Naamani. Siku hizi Mungu hutumia Madaktari kusaidia watu. Mungu ndiye huponya.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Karibisha watoto wanapofika.
2. Imba: "Yesu Husaidia Wagonjwa"
3. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa.
4. Mwulize mtoto mmoja kuchukua chombo cha sadaka. Wengine waanze kutoa sadaka zao wanapo endelea kuimba: "Napenda Kwenda Kanisani".
5. Ita kila jina na uweke alama katika kitabu kwa wale waliohudhuria.
6. Ongea na watoto kuhusu wakati walipokuwa wagonjwa. Uliza, "Nani aliye wasaidia? Mlienda clinic? Je, mmeshawahi kwenda hospitalini? Mlimeza dawa?" Wape watoto muda wa kujibu kila swali.

Waache watoto waige jinsi ya kusaidia. Mtoto mmoja ajifanye



usingizi. Chagua mtoto mmoja awe mfano wa mwezi. Asimame mbele na kushika kichwa chake. Halafu jua lianze tena. Watoto waamke tena. Rudia mara mbili au tatu. Wachague watoto tofauti kuwa jua au mwezi.

6. **Kifungu cha Biblia:** Fungua Biblia yako na usome, "Mungu....wewe hufanya giza kukawa usiku" (Zaburi 104:1,20).
7. Waulize watoto, "Je, nyinyi hufanya nini wakati wa usiku? Kwa nini mnafikiri Mungu aliumba kuwe na usiku? Ndiyo, tunahitaji kulala na kupumzika. Je, nyinyi husikiza kelele za usiku? Nyinyi husikia nini? Hebu tuimbe wimbo kuhusu Mungu."
8. Wimbo: "Mungu Yu Karibu"
9. **Fungua Biblia Yako Katika Mwanzo 28** na usimulie hadithi.

**SAFARI YA YAKOBO**

"Yakobo, Yakobo," Isaka alimwita mwanawe. "Nataka uende safari. Nataka umtembelee Labani."

Labani aliishi katika kijiji kingine. Safari hii ingechukua siku nyingi.

Yakobo alijitayarisha kwenda. Akavaa viatu. Mama yake akampikia chakula. Alipokuwa tayari, baba yake alimwombea ulinzi wa Mungu.

Yakobo alianza safari. Kwanza, alitembea haraka. Halafu jua likawa kali. Baadaye akaanza kuchoka. Akapumzika kidogo. Akala mkate. Akaanza tena kutembea. Jua lilikuwa linakuchwa. Baadaye kukawa usiku. Akaona nyota ya kwanza, halafu nyingine na nyingine. Kukawa giza.

"Nitalala hapa," Yakobo akajiambia. Akaona mahali pazuri pa kulala. Akalalia manyasi. Akaweka kichwa chake juu ya jiwe.

Alipokuwa amelala, akaangalia mbinguni. Akaona nyota na mwezi. Akasikia kelele za usiku. Baadaye akalala usingizi.

Alipokuwa amelala usingizi, aliota ndoto. Katika ndoto hiyo, Mungu alisema naye. Mungu akasema, "Yakobo, niko hapa pamoja nawe. Nitakulinda. Nitakuwa nawe kila wakati."

Yakobo aliamka. Akaangalia kila mahali lakini hapakuwa na mtu. Aliona tu nyota na mwezi. Hakumsikia mtu ye yote.

"Mungu yu nami mahali hapa," akasema. "Atakuwa nami po pote niendapo. Sitaogopa. Mungu ananilinda."

10. Imba: "Najua Mungu Ananitunza"
11. Omba, umshukuru Mungu kwa ulinzi wake kwa kila mtoto.
12. Picha: Waonyeshe picha No. 6. Uliza watoto: "Mtu huyu ni nani? Je, anafanya nini? Anaona nini? Je, anasikia nini?
13. Kifungu cha Biblia: "Hutaogopa hofu ya usiku" (Zaburi 91:5). Eleza kuwa Mungu aliuumba usiku ili tuweze kulala na kupumzika. Hataki sisi kuogopa. Atatutunza. Waulize watoto kusema kifungu hiki. Uliza, "Utafanya nini wakati unapopatwa na woga usiku?" Jadili.
14. Imba: "Yesu Anipenda"
15. Mshukuru Mungu kwa kuumba usiku na kwa ajili ya ulinzi wake wakati wa usiku.



Somo 7

# DHORUBA KUU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu hututunza wakati wa dhoruba.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Ee Bwana. Wewe U karibu" (Zaburi 119:151).

Nyimbo:
"Mungu Yu Karibu"
"Najua Mungu Ananitunza"
"Yesu Anipenda"

Tumia picha Namba 7

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Marko 4:35-41

Wakati mwingine watoto huogopa ngurumo na radi. Huogopeshwa na kelele za mvua kubwa. Wanahitaji msaada wa kushinda woga huu. Hadithi ya Yesu akituliza dhoruba katika Marko 4:35-41 inasema kuwasaidia watoto kuelewa kuwa Mungu yu karibu kila mara.

Dhoruba ni nyingi katika bahari ya Galilaya. Watu waliokuwa na Yesu walikuwa wavuvi. Walijua zaidi kuhusu mashua na dhoruba. Lakini dhoruba hii ilikuwa mbaya mno. Waliogopa.

Yesu akafanya mwujiza. Akatuliza dhoruba hiyo. Alikuwa mwenye uwezo juu ya upepo na mvua. Watu waliokuwa na Yesu wasingekuwa wenye woga. Wangemwamini atawatunza. Baadhi yao walimwamini kwa sababu walimwomba awasaidie. Lakini walikuwa wenye imani kidogo na waliogopa.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Ita kila mtoto kwa jina lake anapofika darasani.
2. Wimbo: "Yesu Anipenda"
3. Chagua mtoto mmoja ashike chombo cha sadaka wakati wengine wanapofika na kutoa sadaka zao. Msaidie aseme, "Asante Mungu kwa sadaka hii."
4. Weka alama (✓) kwa jina la yule aliyehudhuria. Hesabu watoto.
5. Waambie watoto wakae katika mviringo. Mnong'onezee mtoto aliyekaa karibu nawe kuwa "Yesu anakupenda". Mwambie mtoto huyo kunong'oneza neno hilo kwa mwenzake aliye karibu naye. Waendelee vivyo hivyo mpaka kila mmoja asikie habari hiyo na amwelezee mwenzake. Mtoto wa mwisho ataambia kikundi hicho lile alilosikia.



6. Wimbo: "Yesu Anipenda"
7. Waambie watoto kuwa Mungu ameumba vitu vingi sana. Waulize watoto kutaja baadhi yao. Waache wataje vingi jinsi wawezavyo.......... maua, nyasi, watu, miti, wanyama na kadhalika. Taja "Jua." Pengine mmoja atasema "Mvua". Uliza, "Je, mnapenda mvua? Mungu huonyesha upendo wake kwa kutupatia mvua." Eleza kuwa wakati mwingine mvua inaponyesha, upepo huvuma, nguvumo na radi husikika. Lakini Mungu hataki tuogope. Hukaa karibu nasi.
8. Waambie watoto kuwa kuna kifungu cha Biblia kisemacho, "Ee Bwana, wewe u karibu" - (Zaburi 119:151). Sema kifungu hicho pamoja na watoto.
9. Wimbo: "Mungu Yu Karibu"
10. Sema, "Wakati fulani Yesu alikuwa pamoja na wavuvi. Kulikuwa na dhoruba kuu. Sikilizeni hadithi kuhusu Yesu na marafiki zake."
11. **Fungua Biblia yako katika Marko 4** na usimulie hadithi.

## DHORUBA KUU

Yesu alikuwa amechoka. Alihitaji kupumzika. Alikuwa amefundisha mchana kutwa. Alikuwa karibu na bahari ya Galilaya. "Na tuvuke mpaka ng'ambo" akasema. Yeye na wanafunzi wake wakaingia katika mashua. Yesu alikalia kiti cha nyuma. Baadaye akalala usingizi.

Upepo baridi ukaanza kuvuma. Hata nyota na mwezi havikupata kuonekana. Kukawa giza kuu.

Upepo ulikuwa wenye nguvu. Mashua ikapelekwa huku na huko baharini.

Marafiki wa Yesu wakajaribu kupeleka mashua yao ukingoni mwa bahari. Lakini upepo ulikuwa na nguvu. Wakaingiwa na hofu. Dhoruba ikawa mbaya sana.

Maji yakaanza kuingia mashuani. Watu hao wakajua kwamba mashua yao itajaa maji. "Yesu anafanya nini? wakaulizana. Yesu alikuwa amelala usingizi. Lakini upepo huo haukumwamsha.

"Yesu, Yesu," wakaita. "Mashua inajaa maji. Unaweza kutusaidia?"

Yesu akaamka. Akaona maji mashuani. Akahisi upepo. Akaona maji baridi ya mvua usoni mwake. Akainua mikono yake na akasema, "Nyamaza, utulie." Mara moja upepo ukatulia. Mwezi na nyota vikaonekana. Ulikuwa usiku mtulivu.

Marafiki wa Yesu hawakuogopa tena. Walishangaa. Wakatambua kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu.

12. Onyesha watoto picha ya Yesu na wanafunzi wake wakiwa katika mashua. Zungumzia kuhusu picha hiyo. Pengine watoto wanaishi karibu na bahari. Sema nao kuhusu ulinzi wa Mungu kwetu kila mara.
13. Wimbo: "Najua Mungu Ananitunza."
14. Omba, ukimshukuru Mungu kwa ulinzi wake kwetu.